*Kioo cha Lugha, Juz. 20(1), 18-35*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i1.2

# Matumizi ya Sitiari katika Kazi za Fasihi: Mifano kutoka Nyimbo za Kivunjo

*Ernesta S. Mosha*[1]

**Ikisiri**

Makala hii inajadili matumizi ya sitiari kutoka katika nyimbo za Wachaga wa Vunjo. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Mwingiliano (Black, 1962), makala imeweka bayana namna ambavyo sitiari katika kazi za fasihi zinatumika kuugawa, kuupanga na kuueleza ulimwengu. Kwa kutumia data kutoka katika nyimbo tatu za taasisi ya ndoa kutoka katika jamii ya Wachaga wa Vunjo, makala imebainisha kuwa watunzi wa kazi za fasihi huunda sitiari kutoka katika mazingira na maisha halisi ya jamii ambayo wahusika wameyazoea. Pia, sitiari hizo hubuniwa kutoka katika mazingira mahususi ya kiutamaduni hali ambayo inalazimu ufafanuzi wake kuzingatia utamaduni na mazingira husika ili iweze kueleweka. Aidha, imebainika kuwa kupitia sitiari zilizotumika katika nyimbo teule, wanajamii wanafahamishwa namna ya kukabiliana na hali mbalimbali wanazokutana nazo katika maisha. Kwa njia hii, fasihi ina nafasi kubwa ya kubuni mbinu zinazoweza kuleta mabadiliko kwa wanajamii kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

## 1.0 Utangulizi

Lugha ni kifaa muhimu katika kazi za fasihi kwani ndicho hutumiwa na mtunzi katika kuwasilisha kazi yake. Leech (1991) anaeleza kuwa kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vema kama lugha iliyotumiwa haijaeleweka. Kwa hiyo, ni vyema kuchunguza jinsi mtunzi alivyotumia lugha kuwasilisha ujumbe wake kwa wahusika. Carter (1989) anasisitiza kuwa maana katika kazi ya fasihi inapatikana katika lugha, hivyo, kuna umuhimu wa kuchunguza lugha iliyotumika ili kupata maana iliyokusudiwa. Weedon (1997) akifafanua zaidi kuhusu lugha katika kazi za fasihi anaeleza kuwa lugha huumba ulimwengu unaotuzunguka na kutuaminisha yale tunayojua na ambayo hatuyajui. Hii ina maana kuwa lugha inajenga fikra na ushawishi kwa yale yanayokubalika na kuonekana kuwa ni ya kawaida katika jamii. Kwa msingi huu, kupitia fasihi yale ambayo jamii inayaamini husisitizwa, huendelezwa na wakati mwingine hukemewa. Lugha kama kifaa kinachobeba ujumbe katika kazi za fasihi ni kipengele muhimu cha kuchunguza ili kujua namna kilivyotumika katika kazi za fasihi kwa ujumla na hasa katika fasihi

[1] Mhadhiri Mwandamizi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: moshaernesta@yahoo.co.nz

simulizi. Hata hivyo, matumizi ya lugha katika fasihi, hususani fasihi simulizi, hayajajafanyiwa uchunguzi wa kina (Senkoro, 1988; Mulokozi, 2017). Hivyo, ili kupata ujumbe katika kazi za fasihi ni vyema kuelewa matumizi ya vipengele mbalimbali vya lugha vilivyotumika. Besha (1983) anasisitiza kuwa ili kupata ujumbe uliopo katika kazi za fasihi ni muhimu kuchunguza namna mtunzi alivyotumia vipengele mbalimbali vya lugha katika kazi yake. Katika fasihi kuna vipengele anuwai vya lugha kama vile uteuzi wa msamiati, matumizi ya methali na semi na tamathali za usemi (Wamitila, 2010). Hata hivyo, katika makala hii tunachunguza matumizi ya sitiari - aina mojawapo ya tamathali za usemi. Sitiari imeteuliwa kwa kuwa ni tamathali inayotumiwa zaidi na waandishi katika kufasiri na kuelezea ulimwengu unaotuzunguka (Lakoff na Johnson, 2003); hivyo, ni vema kujua namna inavyotumika katika nyimbo za ndoa za Kivunjo ili kupanua wigo wa uelewa wa tamathali hii.

Sitiari ni tamathali kongwe ambayo imeanza kuchunguzwa tangu kipindi cha akina Aristotle. Katika kazi yake maarufu ya 'Poetics', Aristotle anaeleza kuwa sitiari ni tamathali inayotumia jina kutoka kitu kilicho katika kundi lingine. Uhamishaji wa jina unaweza kutoka katika kundi moja la vitu kwenda lingine au kutoka dhana halisi kwenda dhana dhahania (Lan, 2005). Katika uwanja wa fasihi, sitiari hutumiwa sana na waandishi katika kazi zao kutokana na sababu zifuatazo: kwanza, ni tamathali ya usemi ambayo inatumiwa na wasanii kuonesha upekee katika kueleza uzoefu wao katika mazingira yanayowazunguka (Lakoff na Johnson, 2003). Pili, tamathali hii huonesha jinsi binadamu anavyoweza kueleza ulimwengu na mazingira yanayomzunguka kwa kuzingatia ubunifu wa msanii. Tatu, tamathali hii inatumika kueleza ukweli kuhusu maisha kwa maneno machache, yaani jambo ambalo lingeelezwa kwa maneno mengi kwa kutumia lugha ya kawaida huelezwa kwa maneno machache (Almirabi, 2015). Nne, sitiari hufanya dhana dhahania kuwa halisi, huibua hisia na uhalisia kwa wasomaji/wasikilizaji (Kövecses, 2010). Kutokana na manufaa haya ya sitiari, Lakoff na Johnson (2003) wanaweka wazi kuwa sitiari ni tamathali inayotumika kuelewa maisha ya kila siku na ulimwengu unaotuzunguka kwa ujumla. Pamoja na umuhimu wa sitiari katika kazi za fasihi, maana katika sitiari hazipo wazi, jambo linaloweza kuwatatiza wasomaji au wasikilizaji katika kupata maana iliyokusudiwa. Kwa hiyo, ni muhimu wasikilizaji au wasomaji wakajua mazingira sitiari zilimotumika ili waweze kuchambua vipengele vyake hususani kitajwa na kifananishi kwa kuhusisha na mazingira husika. Kutokana na sababu hiyo, makala hii inalenga kuchambua sitiari zilizotumika katika nyimbo teule za ndoa za Kivunjo zinazopatikana katika Wilaya ya Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro.

Makala imegawanyika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza imeeleza umuhimu wa kuchunguza sitiari kama tamathali inayotumiwa na watunzi wa kazi za fasihi katika kufasiri mazingira yanayotuzunguka. Katika sehemu ya pili, tumejadili maana ya sitiari, aina za sitiari pamoja na nadharia za sitiari. Sehemu ya tatu imeweka bayana namna nyimbo zilizotumika katika makala hii

zilivyopatikana na muhtasari wake na kufuatiwa na mjadala wa matumizi ya sitiari katika nyimbo teule kisha kutoa hitimisho.

## 2.0 Sitiari kwa Ujumla

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo inatumiwa sana katika kazi za fasihi, hususani ushairi ambapo nyimbo ni utanzu wake. Ni tamathali inayojengeka kutokana na ubunifu ambao athari yake hutegemea uhamishaji wa maana na hisi kutoka katika kitu au dhana moja hadi nyingine tofauti. Vitu viwili vinavyohusishwa kwa kawaida havina uhusiano wa moja kwa moja (Kahigi na Mulokozi, 1982). Sitiari humsaidia msanii kuumba dhana kwa kuhusisha vitu vilivyomzunguka, alivyoviona au alivyovisikia. Culler (1981) anasema kuwa kwa kutumia sitiari msanii anaonesha ubunifu katika kuipa kazi yake uhai na uhalisi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, wakati msanii anatumia sitiari anahusisha vitu au dhana kutoka katika makundi tofauti ambayo yanafahamika kwa walengwa, hali ambayo humsaidia msikilizaji au msomaji kupata maana inayokusudiwa.

Kwa kawaida, sitiari huwa na sehemu mbili; kitajwa na kifananishi. Kitajwa ni neno linalotajwa kama mada ya sitiari na kifananishi ni neno la kisitiari. Mfano ufuatao unafafanua sehemu hizi za sitiari '*mapenzi ni ua'*. Katika mfano huu, *mapenzi* ni kitajwa na *ua* ni kifananishi. Ua lina sifa zifuatazo: hukua, hupendeza, huvutia, hufifia na hatimaye hufa. Kama lilivyo 'ua', mapenzi ni kitu kinachovutia, hupendeza, hukua na wakati mwingine hufifia na hata kufa. Sifa hizi za ua ndizo zinazofananishwa na mapenzi. Martin (1975) anaeleza kuwa sifa zinazounganisha kitajwa na kifananishi ni za muhimu katika kubaini uzoefu halisi unaoonekana. Lugha inaweza kueleweka vizuri zaidi kupitia uzoefu wetu wa kila siku na ulimwengu unaotuzunguka. Kwa hiyo, kupitia sitiari uhakiki wa lugha unaweza kufanyika kwa kuhusisha maisha ya kila siku na mazingira ya kiutamaduni. Kwa maneno mengine, sitiari inatusaidia kuchagua mambo ya kusisitiza, ya kuacha na kuweka pamoja mahusiano ya nyanja mbalimbali kupitia vitu halisi. Hii inadhihirisha kuwa sitiari ni tamathali muhimu kwa ushairi na masimulizi. Kwa sababu hii, Leech (1991) anasema kuwa sitiari ni tamathali hai inayoumbwa kwenye mawazo ya msanii ili kuhakikisha kuwa ujumbe aliokusudia unawafikia walengwa waliokusudiwa.

### 2.1 Aina za Sitiari

Wataalamu wa lugha na fasihi wameeleza aina mbalimbali za sitiari. Leech (1991) amegawa sitiari katika makundi manne ambayo ni sitiari halisi, sitiari za wanyama, sitiari za binadamu na sitiari za hisia mseto. Pia, ametaja sitiari pana na sitiari changamano kama makundi mengine ya sitiari. Kwa upande mwingine, Wamitila (2003) amegawa sitiari katika makundi tisa. Baadhi ya makundi hayo ni sitiari fiche, sitiari fifi au chakavu, sitiari kuukuu, sitiari sheheno, sitiari thabiti, na kadhalika. Katika makala hii tutatumia aina za sitiari zilizobainishwa na Leech

(1991) - yaani sitiari halisi, sitiari za wanyama, sitiari za binadamu na sitiari za hisia mseto. Aina hizi za sitiari zimeteuliwa kwa sababu zimejitokeza kwa kiasi kikubwa katika nyimbo za Kivunjo zilizochunguzwa katika makala hii.

Sitiari halisi zinaipa uhalisi dhana dhahania, yaani dhana zinaelezwa kwa kutumia vitu halisi. Hii inatokana na msanii kuchagua sitiari ambazo zinamwezesha kueleza ujumbe aliokusudia kwa uhalisi na kwa uwekevu zaidi. Msomaji au msikilizaji huweza kupata ujumbe kwa urahisi kwa kuhusisha dhana dhahania zilizotumika na vitu ambavyo vinapatikana katika mazingira halisi. Mfano mmojawapo ni ule wa *muda ni fedha* (Lakoff na Johnson, 2003). Hapa muda ambayo ni dhana dhahania imehusishwa na fedha.

Aina nyingine ya sitiari, ni sitiari za wanyama. Hizi huvipa sifa za wanyama vitu ambavyo havina sifa hizo. Kwa mfano, ‘*Juma ni simba’*. Kwa upande mwingine, sitiari za binadamu ni aina ya sitiari ambazo kitu ambacho hakina sifa za binadamu kinapewa sifa hizo. Mfano, *‘mdomo ni kigawa ukoo’.* Hapa mdomo umepewa uwezo wa kutenda kama binadamu - uwezo wa kugawa wanaukoo. Kwa kufanya hivyo, wasomaji au wasilikizaji wanaweza kuelewa kwa urahisi madhara ya mdomo kutokana na nguvu ya utendaji uliopewa. Kwa kiasi kikubwa, aina hii ya sitiari inafanana sana na tamathali za usemi za aina ya uhaishaji. Perrine (1987) anaeleza kuwa, uhaishaji siyo aina ya tamathalli za usemi bali ni aina ya sitiari ambayo inapewa sifa za binadamu. Hata hivyo, katika makala hii, tunatumia sitiari za binadamu kama zilivyoelezwa na Leech (1991) ili kuwa na ulinganifu.

Sitiari za hisia mseto ni aina nyingine ya sitiari ambayo inahamisha maana kutoka katika dhana moja kwenda katika dhana nyingine kwa kuzingatia uzoefu na muktadha wa kiutamaduni. Kwa mfano, ‘*mwanamke ni jembe’*. Hapa mwanamke anafananishwa na jembe. Umuhimu wa jembe katika jamii ya wakulima umehamishiwa kwa mwanamke. Katika jamii ya wakulima, jembe ni kifaa muhimu ambacho kina kazi mbalimbali kama vile kulima, kupalilia, kungo’a visiki, na kadhalika na bila jembe huwezi kuendesha shughuli zinazotakiwa. Kwa kuhamisha sifa za jembe na kumpa mwanamke, wasomaji au wasikilizaji wanajua umuhimu wa wanawake katika jamii. Kwa kuchunguza aina hizi za sitiari, tunagundua tabia ya sitiari katika kupambanua mazingira yanayotuzunguka kwa kutumia vitu vilivyopo. Leech (1991:185) anaeleza: “…tunapata dhana ya vitu visivyo na uhai kwa haraka zaidi pale tunapovipa uhai. Vilevile, dhana dhahania zinapata uhalisi pale tunapozipa sifa za vitu halisi vinavyotuzunguka katika mazingira yetu.”

## 2.2 Nadharia kuhusu Sitiari

Katika uwanja wa fasihi, nadharia mbalimbali zimetolewa kuhusu sitiari. Makala hii inatumia Nadharia ya Mwingiliano (Black, 1962). Nadharia ya Mwingiliano inaeleza kuwa sitiari haitumiki badala ya usemi wa kawaida kwa kuwa maelezo ya

kisitiari hayawezi kubadilishwa na maneno mengine, wala vitu vinavyofanana kwa kuwa sitiari hazifungamani na mawazo kuhusu ulimwengu bali zinaeleza jinsi tunavyoweza kuhusisha na kufananisha mawazo haya na ulimwengu halisi (Black, 1962; Lakoff na Johnson, 2003). Kwa hiyo, nadharia hii inaona kuwa sitiari ni sehemu mahususi ya mchangamano wa kazi ya lugha ya kuugawa, kuupanga na kuueleza ulimwengu (Lakoff na Johnson, 2003). Pia, Nadharia ya Mwingiliano inatoa mwanga kuhusu uhalisia wa mazingira yanayoizunguka jamii. Katika muktadha huu, sitiari huangaliwa kama uhamishaji wa kimaana kutoka kwenye kiima kidogo kwenda kwenye kiima kikuu (Wamitila, 2003). Hii ina maana kuwa msomaji au msikilizaji anaunganisha maana ya picha iliyoundwa na msanii na maana ya msingi ili kupata wazo linalowakilishwa (Culler, 1981). Kwa kutumia nadharia hii tunaweza pia kueleza kuhusu sehemu mbili za sitiari, kitajwa na kifananishi. Kwa kutumia mfano wa '*Julita ni jua'.* Julita ni kitajwa na jua ni kifananishi ambacho sifa zake za joto na kung'aa zimehamishiwa kwa Julita. Hii ni kutokana na wasomaji au wasikilizaji kuwa na maarifa kuhusu jua na hivyo kuweza kuhusisha maarifa hayo katika kumwelezea Julita. Lakoff na Johnson (2003) wanatoa mifano kadhaa katika kufafanua dhana dhahania kwa kutumia sitiari. Wanaeleza kuwa ni rahisi kuelewa sentensi zifuatazo kwa kuhusisha na mambo halisi yaliyopo katika mazingira halisi:

1. Muda ni fedha. 2. Muda ni raslimali adimu. 3. Muda ni bidhaa adimu[2].

Katika sentensi hizi Lakoff na Johnson (2003) wanabainisha kuwa dhana ya muda, msingi wake unaeleweka vyema kutokana na kuhusisha na vitu kama fedha, rasilimali na bidhaa. Muda ni fedha inaweka bayana umuhimu wa muda kama fedha zilivyo muhimu kwa wanajamii. Aidha, wasomaji au wasikilizaji wanajua matumizi ya rasilimali na bidhaa mbalimbali kwa jamii husika. Hivyo, dhana hizi halisi zinapotumika zinarahisisha kuhusisha muda na shughuli za kila siku za mwanadamu katika mazingira halisi.

Upekee wa maana zinazoambatishwa katika sitiari ni matokeo ya mwingiliano kati ya kitajwa na kifananishi (muda na fedha). Kwa kiasi kikubwa, ubora wa sitiari unategemea uwezo wa wasomaji au wasikilizaji kuweza kubaini sifa pambanuzi kati ya kitajwa na kifananishi kulingana na mazingira. Katika makala hii, tunatumia nadharia hii ya Mwingiliano ili kubaini uhusiano kati ya dhana zilizotumika kitaswira na zile zilizotumika kawaida ili kupata maana iliyokusudiwa katika nyimbo teule zilizotumika katika makala hii.

## 3.0 Methodolojia

Sehemu hii inaeleza methodolojia iliyotumika kupata nyimbo zilizotumika katika makala pamoja na kutoa muhtasari wa nyimbo hizo ili kumwezesha msomaji kuelewa kwa urahisi.

[2] Mifano hii imetolewa kwa lugha ya Kiingereza. Tafsiri ni ya mwandishi.

**3.1 Methodolojia Iliyotumika Kupata Nyimbo Zilizotumika**

Makala hii imetumia nyimbo kutoka kabila la Wachaga wanaopatikana kaskazini mwa Tanzania katika mkoa wa Kilimanjaro. Hata hivyo, Wachaga hawaongei lugha moja. Nurse (1977) anabainsiha makundi makubwa matatu yanayoendana na maeneo ya kiutawala ya zamani ambayo ni Vunjo, Hai na Rombo. Makala hii imetumia nyimbo kutoka kwa Wachaga wa Vunjo.

Nyimbo zilizotumika katika utafiti huu zilikusanywa kutoka kwa wazee watano wa jamii ya Vunjo ambao wanaongoza nyimbo katika shughuli mbalimbali za jamii. Jumla ya nyimbo kumi na tano zilikusanywa ambapo nyimbo tatu zenye aina mbalimbali za sitiari kama zilivyobainishwa na Leech (1991) ndizo zilizotumika katika makala hii. Nyimbo zilizoteuliwa ni zile zinazotumika katika shughuli za ndoa - taasisi inayothaminiwa sana na jamii ya Wachaga kwa kuwa inaonekana kuwa ni msingi wa jamii (Stahl, 1969). Kupitia nyimbo hizi, wanandoa wanapewa ushauri na mawaidha kadha wa kadha ili kuhakikisha kuwa wanaendelea vyema. Stahl anafafanua kuwa katika jamii ya Wachaga inaaminika kuwa kuyumba kwa taasisi ya ndoa ni mwanzo wa matatizo mengi katika jamii. Makala hii imetumia nyimbo tatu zinazotumika katika mchakato mzima wa shughuli za harusi za jamii ya Wachaga wa Vunjo. Nyimbo hizo ni: ‘Wenye Ng’ombe’ (*Wenyi Umbe*), ‘Sala ya Ndoa’ (*Kiterewo kya Wolyi*) na ‘Muungano’ (*Kisanza*).

**3.2 Muhtasari wa Nyimbo Zilizotumika**

Wimbo wa kwanza, “Wenye Ng’ombe” (*Wenyi Umbe*) huimbwa na ndugu wa upande wa bibi harusi. Wimbo huu unaeleza umuhimu wa bibi harusi katika familia yake na jamii kwa ujumla. Wimbo huu unabainisha shughuli mbalimbali anazofanya bibi harusi katika familia alikozaliwa na kuwa kuondoka kwake kunaacha pengo. Wimbo wa pili, “Sala ya Ndoa” (*Kiterewo kya Wolyi*) unaimbwa na ndugu wa bwana harusi, ukilenga kuwaombea baraka kwa Mungu na mizimu (mababu) wanandoa wapya. Pia, wimbo unawaelimisha na kuwatahadharisha wanandoa wapya kuhusu changamoto za maisha ya ndoa. Wimbo wa tatu, ‘Muungano’ (*Kisanza*) unaimbwa pia na ndugu wa bwana harusi, ukieleza umuhimu wa maisha ya ndoa katika jamii na jinsi mwanamke na mwanamume wanavyotakiwa kuishi katika ndoa.

**4.0 Matumizi ya Sitiari katika Nyimbo za Wachaga wa Vunjo**

Wachaga wa Vunjo ambao nyimbo zao zimetumika katika makala hii, ni miongoni mwa makabila zaidi ya 120 yaliyopo Tanzania (Muzale na Rugemalira, 2008). Kabila hili linatumia lugha tatu ambazo ni Kivunjo, Kihai na Kirombo. Guthrie (1967) na Nurse (1977) wanaeleza kuwa lugha hizi zinatokana na mgawanyo wa kiutawala uliokuwapo ambao ulikuwa wa maeneo matatu – Vunjo, Hai na Rombo.

Makala hii imetumia nyimbo za Wachaga wa Vunjo ambao wanapatikana katika maeneo ya Kirua, Kilema, Marangu, Mamba, Mbokomu, Mwika na Uru.

Katika fasihi simulizi, nyimbo ni sehemu muhimu ya maisha ya wanajamii. Katika jamii nyingi za Kiafrika, fasihi simulizi inaakisi hali halisi hususani watu wanavyoishi, wanavyofikiri na kuamini. Aidha, katika mchakato wa kujifunza maarifa ya jamii, vitu vinavyotumika katika jamii kama vile vifaa vya shughuli za kiuchumi, mifugo na mimea hutumika katika kueleza mahusiano changamani ya kijamii kwa urahisi zaidi (Vansina, 1985; Chesaina, 1995). Akisisitiza umuhimu wa fasihi simulizi kwa jamii, Chesaina anaeleza kuwa fasihi simulizi ni nafsi hai ya utamaduni na pia ni kifaa muhimu cha kuhifadhi tunu za jamii. Kupitia fasihi simulizi tunapata taswira na mtazamo wa wanajamii kuhusu maisha yao ya kila siku. Kwa hiyo, kupitia nyimbo za Kivunjo, tunajifunza yale ambayo jamii hii inaamini na mtazamo wa wanajamii kuhusu maisha yao ya kila siku kwa kuchunguza aina mbalimbali za sitiari zilizotumika. Ufuatao ni uchambuzi wa nyimbo teule kuhusu matumizi ya aina mbalimbali za sitiari.

Katika wimbo wa "Wenye Ng'ombe" (*Wenyi Umbe*) ambao unaimbwa na ndugu wa bibi harusi wanapowasindikiza maharusi ukumbini, neno ng'ombe limetumika kisitiari kumwakilisha msichana. Ubeti ufuatao unathibitisha dai hili:

| | |
|---|---|
| *Wenyi umbe nyiso* | Sisi ni wenye ng'ombe |
| *Kocheruo umbe yaru* | Umechukua ng'ombe wetu |
| *Kolura kuro* | Umetuacha hivyo |
| *Kwi uiruo ngesa*? | Hivi unampeleka wapi? |

**Chanzo:** "Wenye Ng'ombe": Ubeti wa 1[3]

Katika ubeti huu mstari wa kwanza na wa pili, msichana anafananishwa na ng'ombe (*umbe*). Mazingira ya sitiari hii yanaonesha kuwa umuhimu wa msichana katika jamii unafananishwa na umuhimu wa ng'ombe. Katika jamii ya Wachaga, ng'ombe ni mnyama anayewapatia wanajamii maziwa, mafuta, nyama, ngozi na mbolea. Ukiwa na ng'ombe unaweza kuuza mazao yake na kupata fedha. Umuhimu huo ndio unaohusishwa na msichana katika familia na kuondoka kwake kunaifanya familia kukosa huduma alizokuwa anatoa kama ambavyo ukiwa huna ng'ombe huwezi kupata mazao yake. Umuhimu wa msichana unafafanuliwa zaidi katika ubeti ufuatao:

| | |
|---|---|
| *Noruo ishami laru* | Umechukua kotama letu |
| *Noruo mara waru* | Umechukua majani yetu |
| *Kwi uruo ngwi zaru?* | Unapeleka wapi kuni zetu |
| *Kwi uruo mawako waru?* | Unapeleka wapi mikono yetu? |

[3] Katika wimbo wa "Wenye Ng'ombe", huu ni ubeti wa kwanza. Mtiririko huu utatumika kutofautisha wimbo mmoja na mwingine na kuonesha idadi ya beti zilizotumika katika wimbo husika.

| | |
|---|---|
| *Kwi uruo ikumbi laru* | Unapeleka wapi jembe letu? |
| *Kwi uruo mringa woru* | Unapeleka wapi maji yetu? |

**Chanzo:** "Wenye Ng'ombe": Ubeti wa 2

Kutokana na ubeti huu, kotama (*ishami*), kifaa kinachotumiwa kukata nyasi kinafananishwa na msichana. Hiki ni kifaa muhimu kwa kuwa nusu ya ng'ombe walio katika jamii hii wanatunzwa ndani na kulishwa kwa kukatiwa nyasi (Dundas, 1968).

Pia, katika mstari wa pili umuhimu wa majani (*mara*) kwa mifugo kama ng'ombe, mbuzi na kondoo unahamishiwa kwa msichana. Katika mstari wa tatu kuni (*ngwi*) ambazo ni chanzo cha nishati katika jamii hii zinatumika kuwafahamisha zaidi wasikilizaji au wasomaji umuhimu wa huyu msichana.

Katika mstari wa nne wimbo unaendelea kusisitiza umuhimu wa msichana kwa kumfananisha na mikono (*mawoko*) ya binadamu. Kwa kawaida ni vigumu kufanya kazi mbalimbali kama huna mikono, hivyo, ni vigumu kuweza kujitegemea. Katika ubeti huu inadhihirisha wazi kuwa pale msichana anapoondoka katika familia na kuolewa, anaacha pengo kubwa. Aidha, umuhimu wa jembe (*ikumbi*) unasisitiza nafasi ya msichana katika familia, kama jembe lilivyo kwa wakulima katika jamii zinazotegemea kilimo. Pia, umuhimu wa msichana katika familia yake ya kuzaliwa unashadidiwa kwa kumlinganisha na maji (*mringa*) kwa viumbe hai.

Katika mifano iliyojadiliwa hapo juu, kizungumzwa ni msichana na kifananishi ni vitu vyote vilivyotajwa; kotama (*shami*), majani (*mara*), kuni (*ngwi*), mikono (*mawoko*), jembe (*ikumbi*) na maji (*mringa*). Sifa zilizojitokeza kati ya msichana na vitu vilivyotajwa ni kiungo cha sitiari. Kwa kutumia vitu hivyo ambavyo vinafahamika katika mazingira ya jamii ya Wachaga, wasikilizaji au wasomaji wanaweza kuelewa umuhimu wa msichana katika familia anayotoka. Ubeti unaofuata unafafanua ni msichana wa aina gani anayeolewa:

| | |
|---|---|
| *Lokunenga tawo* | Tumekupa mfarika[4] |
| *Kopfo zapfo kilele* | Sasa kwako watakuwa wengi |
| *Ambia necha tawoyi* | Mtunze vizuri huyu mfarika |
| *Ifare handupfo* | Hana kovu |

**Chanzo:** "Wenye Ng'ombe": Ubeti wa 3

Katika ubeti wa tatu wimbo unaweka bayana kuwa kilichotolewa ni kitu kizuri, 'tumekupa mfarika' (*lokwinenga tawo*), ikimaanisha kuwa kiko katika hali nzuri, chenye nguvu na afya nzuri, safi kabisa–bikira. Katika kueleza umuhimu wa bibi harusi kuwa bikira, katika jamii ya Wachaga, Marealle (2002:51) anasema:

---

[4] Mfarika ni mnyama ambaye ameshakua lakini bado hajazaa (TUKI, 2019).

> Jamii ya Wachaga ni jamii ambayo inaamini sana miiko, hivyo msichana bikira ndiye anayepewa ndoa ya kimila na wanaomhusu na kupewa mafundisho ya aina mbalimbali. Hivyo, msichana bikira ni heshima kwa wazazi wa pande zote mbili.

Pia, katika jamii hii, watu wanaweza kuazima mfarika, malipo yake yakiwa ni mbolea kwa siku za mwanzo na anapozaa anapata maziwa na mafuta. Ndama wanaozaliwa wa kwanza anachukua mmiliki wa ng'ombe na ndama wa pili anakuwa ni wa yule aliyeazimwa mfarika. Mpangilio huu wa kugawana ndama wanaozaliwa ni wa kawaida na unaendelea mpaka sasa. Kwa utaratibu huu, aliyeazima mfarika akifanya kazi kwa bidii anapata ng'ombe wake kutokana na kugawana ndama wanaozaliwa. Hali hii inawafanya Wachaga wanaofanya kazi kwa bidii hata kama awali walikuwa hawana kabisa mifugo waweze kupata mifugo na kuanza kuwaazima wengine. Kwa hiyo, msichana anayeolewa anafananishwa na aina hii ya ng'ombe ambayo ina manufaa makubwa kwa jamii ya Wachaga.

Ubeti wa nne katika wimbo huu wa "Wenye Ng'ombe" unaeleza aina ya ushirikiano ulioundwa baada ya koo mbili, yaani ukoo wa bwana harusi na wa bibi harusi kuungana kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| *Kochelupfunga na lelema* | Umetufunga na *lelema*[5] |
| *Nolupfungyia uwangonyi* | Umetufungia katika *uwango*[6] |
| *Kyikyi ulemanyia yamngana* | Ulijuaje ameshakuwa mkubwa |

**Chanzo:** "Wenye Ng'ombe": Ubeti wa 4

Katika ubeti wa nne hapo juu neno '*lelema*' limetumiwa kuonesha umuhimu wa ushirikiano ulioundwa kati ya koo mbili zilizounganishwa kwa ndoa ya watoto wao. Kamba aina ya '*lelema*' inatumika katika jamii ya Wavunjo kufunga kitovu cha mtoto anapozaliwa kwa kuwa inaaminika kutoa dawa inayosaidia kuponyesha kitovu cha mtoto mchanga. Kwa hiyo, kamba hii ni muhimu sana kwa jamii ya Wachaga wa Vunjo. Kwa kutumia aina hii maalumu ya kamba, umuhimu wa ushirikiano kati ya koo mbili zilizoungana unabainishwa. Aidha, katika kusisitiza kuwa ushirikiano huu ni wa kudumu, *uwango*, kifaa kinachotumiwa kufungia wanyama hususani ng'ombe kinatumika.

Katika kuendelea kusisitiza umuhimu wa ndoa katika jamii ya Wachaga wa Vunjo, wimbo wa "Sala ya Ndoa" (*Kiterewo kya Wolyi*) ambao unatumika kuwaombea baraka maharusi, katika ubeti wa kwanza unabainisha thamani ya

---

[5] Aina ya kamba inayotumiwa na wakunga wa jadi katika jamii ya Wavunjo kufunga kitovu cha mtoto anapozaliwa.

[6] Nguzo zinazotumiwa kufungia ng'ombe katika nyumba za asili za Wachaga.

wanandoa kuwa wameumbwa kwa mfano wa Mwenyezi Mungu na hivyo wanawapokea kwa furaha na kumwombea bwana harusi ulinzi:

| | |
|---|---|
| *Nulelunenga shuma* | Ulitupa mifugo |
| *Shifananyi naiyo* | Wanaofanana na wewe |
| *Mndumii Rywa warilyia p*ungai | Mwenyezi Mungu pokea hili fahali |
| *Uliringe* | Ulilinde |

**Chanzo:** "Sala ya Ndoa": Ubeti wa 1

Katika jamii ya Wachaga, mifugo (ng'ombe, mbuzi, kondoo) ni kitu cha manufaa na kipimo cha umaarufu. Katika ubeti wa kwanza wa wimbo wa 'Sala ya Ndoa' hapo juu, tunagundua kuwa umuhimu wa mifugo umehamishiwa kwa watoto. 'Fahali' katika mfano huu, ametumika kuwakilisha bwana harusi. Kwa kawaida, fahali huwekwa katika sehemu yake ambapo analishwa kwa muda kwa lengo la kuchinjwa kwa ajili ya karamu au sadaka kwa miungu (Dundas, 1968). Kwa hiyo, tunaona kuwa heshima hii ndiyo inayohamishiwa kwa bwana harusi kwamba wanamwomba Mwenyezi Mungu amlinde.

Wimbo huu pia unafafanua nafasi ya taasisi ya ndoa katika jamii, kwa kuweka bayana mafunzo anayopewa mwanamume anapooa. Mfano ufuatao unaweka bayana:

| | |
|---|---|
| *Meku lokualikyia* | Kijana tumekupa mke |
| *Uwokye manya* | Lazima uelewe |
| *Mndumka nyi mana* | Mwanamke ni mtoto |
| *Nyi iwache lapfo* | Ni ndama wako |
| *Ma ulalyisepfuo* | Usimnyanyase |
| *Lyiweiye mando ng'a moondinyi* | Lazima umlishe vizuri |

**Chanzo:** "Sala ya Ndoa": Ubeti wa 2

Katika mfano ulionukuliwa hapo juu, 'mwanamke ni mtoto' (*mndumka nyi mana*). Hili ni jambo ambalo limezua mjadala miongoni mwa wanaharakati kwa kuona kuwa mwanamke anafananishwa na mtoto, yaani ni mtu anayehitaji uangalizi, kulelewa, ni mtu tegemezi, na kadhalika. Kwa upande mwingine, tunaona kuwa mtoto anathaminiwa, anaaminika, anapendwa, na kadhalika. Sifa hizi ndizo zinazohamishwa kutoka kwa mtoto na kupewa mwanamke. Kwa hiyo, jamii inategemea mume amthamini, ampende na amwamini mke wake. Kutokana na sifa hizi tunarejelea mawazo ya Martin (1975) kuwa katika kubainisha sifa zinazounganisha kitajwa na kifananishi ni lazima kuwa makini katika kubainisha sifa zilizokusudiwa kulingana na mazingira.

Vilevile, katika ubeti huu mwanamume anaaswa kuwa ni lazima amtunze mke wake. Jambo hili linasisitizwa kupitia maneno 'ni ndama wako' (*nyi iwache lapfo*). Huduma anazopewa ndama ni tofauti na wanazopewa wanyama wakubwa. Kwa hiyo, mambo anayofanyiwa mnyama huyu mdogo zimehamishiwa kwa mke. Aidha, katika kuangalia matumizi ya sitiari hii ni vema tukaangalia jamii

inayohusika, na kuona ni jinsi gani inavyofanya mambo mbalimbali. Kwa mfano, utunzaji wa mwanamke katika jamii hii ni jambo ambalo linasisitizwa sana. Kutokana na hali hiyo tunaona kuwa wimbo huu unaunda sitiari kwa kuchota mambo yaliyopo katika jamii ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Kwa hiyo, tunagundua kuwa jamii ya Wachaga wa Vunjo haina lengo la kumdunisha mwanamke na kumwona kuwa ana akili za kitoto au ni tegemezi kupitia wimbo huu, bali azma ni kuonesha umuhimu wake katika jamii na mambo anayostahili kufanyiwa.

Wazo hili la kumpenda na kumtathimini mke linafafanuliwa pia na Robert (1966) katika "Utenzi wa Adili". Katika utenzi huu, Robert anamshauri mwanawe ampende na kumheshimu mke wake kama mama yake. Tena anasisitiza kuwa asimfanyie vurugu. Anasema haya katika ubeti wa 59 na 62 mtawalia:

| | |
|---|---|
| Sita ukioa mke | Mkeo mpe heshima |
| Kwa mapenzi mshike | Mheshimu kama mama |
| Simfanyie makeke, | Mzaa watoto wema, |
| Ila akuanze yeye | Ulivyozaliwa wewe |

Robert (1966:30-31)

Kwa upande mwingine, wazee wanamwomba Mungu awasaidie hawa wanaoingia katika taasisi ya ndoa. Yumkini ni kutokana na wanandoa kutoka katika familia tofauti na sasa wanatakiwa kuishi pamoja. Katika kuomba, maneno yanayotumiwa yanachora picha halisi katika mawazo ya wasikilizaji. Ubeti ufuatao unabainisha hali hii:

| | |
|---|---|
| *Lukuichi Ruwa mrigyi oru* | Tunakujua Mungu mlinzi wetu |
| *Mlunga nguru na pata* | Unayeunganisha msitu na jangwa |
| *Oiyo Ruwa magyi oru loi* | Wewe ni Mungu wetu kweli |
| *Lukuana nekuolokyia* | Tunakusifu na kukunyenyekea. |

**Chanzo:** "Sala ya Ndoa": Ubeti wa 3

Katika ubeti wa tatu wa "Sala ya Ndoa", kwa maneno 'msitu na jangwa' msanii anayapa uhalisia mambo anayoeleza. Hapa anaweka bayana uwezo wa Mungu wa kuunganisha sehemu mbili ambazo ni tofauti kabisa. Hii inaweka wazi kuwa anaweza kuwaunganisha wanandoa waliozaliwa na kulelewa katika mazingira tofauti. Wachaga wanaamini kwamba Mungu ni mkuu kuliko mizimu yote wanayoitambikia na tambiko analotolewa Mungu ni tofauti na tambiko la mizimu (Marealle, 2002).

Aidha, kwa kutumia maneno haya, mtunzi anatuonesha tabia mbalimbali walizonazo binadamu katika jamii. Neno 'msitu' hapa linamaanisha sehemu yenye rutuba, mimea mingi, mvua, na kadhalika, kinyume na jangwa. Msanii ametumia neno 'msitu' kuonesha watu wazuri katika jamii na neno 'jangwa' watu wabaya. Aidha, ametumia maneno haya kuelezea jinsi watu wanavyoweza kujifunza

mambo mema kutoka kwa watu wazuri na kuwa waangalifu pale wanapokuwa na kundi ambalo lina tabia tofauti.

Wimbo huu unaendelea kumtahadharisha bibi harusi kuwa tamaa ni kitu kibaya katika maisha. Unamhimiza kufanya kazi kwa bidii ili aweze kumudu maisha yake. Mfano ufuatao unadhihirisha hoja hii:

| | |
|---|---|
| *Molalange umbe ngamo* | Usikimbilie ng'ombe anayekamuliwa |
| *Maruwa nyi kyirundio* | Maziwa ni kazi |
| *Molakunde shiorie* | Usipende vilivyo tayari |
| *Ulangyi nyi kyowo umanye* | Ujue tamaa ni gurudumu |
| *Pfurukana shavo* | Fanya kazi kwa bidii. |

**Chanzo:** "Sala ya Ndoa": Ubeti wa 4

Katika mfano huu, maneno 'usikimbilie ng'ombe anayekamuliwa' yanatahadharisha kuhusu tabia ya kupenda vitu vilivyo tayari. Badala yake msanii anasisitiza kufanya kazi kwa bidii ili kupata mali/utajiri. Ili hoja hiyo ieleweke vizuri, wimbo umeweka bayana kuwa, 'maziwa ni kazi'. Hapa maziwa yanafananishwa na utajiri. Kwa hiyo, ili kupata utajiri ni lazima kujibidiisha katika utendaji kwa kila jambo unalofanya. Sitiari hii imetumiwa kuonesha kuwa ili ng'ombe aweze kutoa maziwa mengi na mazuri ni lazima alishwe chakula cha kutosha na kinachofaa. Ni lazima tukumbuke kuwa watu wa jamii hii wanatumia vyakula mbalimbali vinavyopatikana katika mazingira yao kama vile nyasi na migomba katika kulishia ng'ombe. Kwa hiyo, ili ng'ombe atoe maziwa yanayofaa ni lazima ujue aina ya nyasi zinazotakiwa na aina ya migomba kwani si kila aina ya nyasi au migomba inafaa kumlisha ng'ombe.

Pia, katika mfano huu tamaa imefananishwa na gurudumu. Kwa kawaida, gurudumu linapozunguka huwa kunakuwa na mabadiliko, linaweza kwenda kasi na kukufikisha sehemu ambayo hukutarajia kama lisipodhibitiwa. Hapa bibi harusi anaonywa kuwa ni lazima kutawala tamaa ili isije ikampeleka sehemu ambayo ni mbaya, hivyo, ni lazima awe mwangalifu. Kwa hiyo, katika maisha ni lazima kufanya kazi kwa bidii na kujenga tabia ya kujitegemea badala ya kutegemea kupewa mali na watu wengine. Buliba na Kamau (2016) wanafafanua kuwa kutowajibika ipasavyo kwa wanandoa husababisha migogoro kwenye familia ambayo isipodhibitiwa huweza kuwa chanzo cha wanandoa kuachana na familia kusambaratika.

Mbali na wanandoa kufanya kazi kwa ujumla, wimbo wa "Muungano" (*Kisanza*), ambao pia unaimbwa na ndugu wa bwana harusi, unaangazia ulazima wa mwanamke kufanya kazi katika maisha ya ndoa. Ubeti ufuatao unafafanua:

| | |
|---|---|
| *Mana owaka wambuye* | Msichana uwe mwangalifu |
| *Uroko nyi ndore* | Uvivu ni ugonjwa |
| *Mawoko nyi kyirundio* | Mikono ni kazi |
| *Mndumka nyi ikumbi* | Mwanamke ni jembe |

| | |
|---|---|
| *Mka nyi kyimndo* | Mke ni kyimndo[7] |

**Chanzo:** “Muungano”: Ubeti 1

Katika mfano huu, uvivu unafananishwa na ugonjwa. Hapa ina maana kuwa madhara yanayotokana na uvivu ni sawa na yale yanayoikumba jamii kutokana na ugonjwa fulani. Kutokana na madhara ya uvivu katika jamii, mwanamke anaonywa kuuepuka. Comer (1995) anashadidia kuwa kujitegemea hufanya akili ya mtu kufikiri zaidi na kuwa na namna mbalimbali za kuweza kujipatia kipato cha kuendeshea maisha yake. Umuhimu wa wanawake kufanya kazi na kujitegemea umewekwa pia bayana na Robert (1966) katika “Utenzi wa Adili”. Robert anasema haya katika ubeti wa 89:

Raha ya uvivu mbaya
Umaskini huzaa
Acha kuikaribia
Usisikize witoe
Robert (1966:34)

Katika mfano huu, Robert anamwonya mwanawe aepuke uvivu. Hii ni dhahiri kuwa katika jamii uvivu ni jambo linalopigwa vita kwa kuwa ni adui wa maendeleo. Aidha, umuhimu wa mwanamke kufanya kazi unasisitizwa kwa kutumia vitu mbalimbali vinavyotumiwa na wanajamii, mathalani, inaelezwa katika wimbo huu kuwa ‘mwanamke ni jembe’ na ‘mwanamke ni *kyimndo*’. Hapa umuhimu wa vifaa hivi kwa jamii ya Wachaga unawapa mwanga wasikilizaji au wasomaji kuelewa umuhimu wa mwanamke kufanya kazi kwa ajili ya mume wake, watoto na jamii kwa ujumla. Kwa upande mwingine, wimbo huu wa “Muungano”, unaeleza madhara ya mdomo kwa jamii kama ubeti huu unavyoweka bayana:

| | |
|---|---|
| *Kyindo kyingi monoko* | Jambo lingine mwanangu |
| *Rumbu nyi kipara mri* | Mdomo unagawa ukoo |
| *Ulamlyiambia lekuokya* | Usipokuwa mwangalifu utakuchoma |

**Chanzo:** “Muungano”: Ubeti 2

Katika mfano huu, wimbo huu unaeleza kuwa ‘mdomo unagawa ukoo’. Hapa mdomo umepewa uwezo wa kutenda au kufanya kazi kama binadamu. Sitiari hii inaonesha kuwa mdomo unaweza kuleta madhara makubwa katika jamii endapo wanajamii hawatakuwa makini katika kutumia midomo yao. Aidha, katika ubeti huu inaelezwa kuwa usipokuwa mwangalifu katika matumizi ya mdomo,

[7] Ni aina ya kisu kinachotumiwa na wanawake katika jamii ya Wachaga kumenyea ndizi, kukatia nyasi, kutolea majani bustanini, katika shamba la maharagwe n.k. (Tafsiri ya mtafiti kwa kuwa ni mmilisi wa Kivunjo).

madhara yake yatakuwa makubwa zaidi; 'utakuchoma'. Hapa mdomo umepewa sifa nyingine ya utendaji, kuweza kuchoma. Madhara anayopata binadamu kutokana na moto yamefananishwa na yale ya mdomo. Kupitia sitiari hii, msikilizaji anapata picha halisi ya namna mdomo unavyoweza kuleta uharibifu kama moto unavyosababisha uharibifu katika mazingira ya binadamu. Hoja hii imeelezwa pia na Robert (1966), katika 'Utenzi wa Adili' ubeti wa 40 anaposema:

Nne fanya taaluma,
Ya kujifunza kusema,
Neno linachoma,
Bila udhuru usitoe.
Robert (1966:28)

Kwa kuchunguza namna wimbo wa 'Muungano' ulivyoeleza kuhusu madhara ya mdomo, na hivyo kushadidia hoja za Robert (1966) kuhusu matumizi ya mdomo tunagundua kuwa katika jamii lugha nzuri ni njia ya kuleta amani na furaha. Hapa tunaweza kuongeza, methali ya Kiswahili, 'Maneno mazuri humtoa nyoka pangoni'. Hapa ikiwa na maana kuwa kutokana na maneno mazuri unaweza kupata jambo lililofichwa mbali ambalo isingekuwa rahisi kulipata.

Kwa upande mwingine, wimbo huu wa 'Muungano' unasisitiza namna ambavyo mwanamke anatakiwa kuishi na mume. Katika wimbo huu, imeelezwa kuwa mwanamke ni mwalimu ambaye anatakiwa kumwelewa mwanafunzi wake, hivyo kuweza kumfundisha mambo mbalimbali kama mfano ufuatao unavyoeleza:

| | |
|---|---|
| *Monoko nopata mii* | Mwanangu umempata mume |
| *Ramia nao kipuo* | Ishi nae vizuri |
| *Nyi mana alaichi kurero* | Ni mtoto asiyejua kuongea |

**Chanzo:** "Muungano": Ubeti 3

Katika mfano huu uliotolewa hapo juu, mume anaelezwa kuwa ni 'mtoto asiyejua kuongea', hivyo, mke anatakiwa amfundishe jinsi ya kuongea. Hapa mwanamume amefananishwa na mtoto. Endapo mama atamfundisha mtoto lugha isiyofaa, mtoto atatumia lugha hiyohiyo. Lakini kama atamjengea msingi mzuri mtoto wake tangu mwanzo, ni dhahiri kuwa atakuwa na lugha nzuri. Swali la kujiuliza ni lugha gani ambayo mke anatakiwa kumfundisha mume ili aweze kuitumia? Hapa wimbo unabainisha kuwa kama alivyo mtoto mambo hupelekwa taratibu siyo kwa pupa. Kwa hiyo, kama ni marekebisho basi siyo kwa siku moja bali ni kitendo cha taratibu kama mtoto anavyojifunza lugha. Ni wazi, katika jamii hii inasisitizwa wanandoa kuchukuliana kwani katika muktadha tofauti wote ni watoto. Hii inadhihirika kwa kuwa mwanamke anaelezwa kuwa mume ni

mtoto ambaye hajui kuongea na mwanamume anaambiwa kuwa mke ni mtoto anayetakiwa kulelewa.

Jambo lingine lililowekwa wazi katika wimbo huu wa "Muungano" ni ugumu uliopo katika maisha ya ndoa. Wimbo huu siyo kwamba unawatisha wale wanaotaka kuingia katika taasisi hii, bali ni angalizo kuwa kwenda kuishi katika familia au jamii tofauti siyo jambo rahisi kutokana na tofauti za tabia, malezi, mila na desturi na kadhalika. Mfano ufuatao unaweka bayana suala hili:

| | |
|---|---|
| *Kyendi umanye* | Ni lazima ujue |
| *Kowandu nyi kyimango* | Kuishi na watu ni kyimango[8] |
| *Ambia necha kisanzakyi* | Ulinde sana muungano huu |
| *Kyilaparakane* | Usivunjike |

**Chanzo:** "Muungano": Ubeti 4

Ubeti huu unaeleza wazi kuwa kuishi na watu ni kazi ngumu. Ugumu wa kuishi na watu wengine unafananishwa na mti wa '*kyimango*'. Mti huu umetumiwa ili kueleza wanandoa wapya kuwa maisha ya ndoa siyo lelemama. Ili kuishi na watu, uvumilivu ni kitu ambacho hakikwepeki. Mfano uliotolewa, unatoa picha halisi kuwa wale wanaoingia katika taasisi hii muhimu, wanatakiwa kuandaliwa vema ili kupata mbinu mbalimbali za kutatua matatizo watakayokutana nayo kwa lengo la kulinda na kuendeleza ndoa. Katika jamii ya Wachaga wa Vunjo, bibi harusi hupewa mafundisho kuhusu maisha mapya anayokwenda kuishi, mafundisho hayo huitwa '*Urawano*' (Marealle, 2002). Kwa hiyo, tunaona kuwa kuna umuhimu wa kuendeleza mafundisho haya ili kuwapa wanandoa wapya maarifa. Pia, inashauriwa kuwa ili mwanamke awe na maarifa yanayofaa anapoingia katika ndoa; anatakiwa kuandamana na watu wenye tabia nzuri. Kwa hiyo, mwanamke anaaswa asiandamane na watu wapumbavu kama inavyoeleza katika mfano huu:

| | |
|---|---|
| *Molasanze na masembo* | Usiandamane na wapumbavu |
| *Kosanza nagho* | Ukiandamana nao |
| *Nochiwa mbulugha* | Utakuwa *mbulugha*[9] |

**Chanzo:** "Muungano": Ubeti 5

Katika ubeti huu, inaelezwa kuwa endapo mwanamke ataandamana na watu wapumbavu yeye atakuwa *'mbulugha'*. Ubeti huu unaweka wazi kuwa endapo mwanamke aliyeolewa atashirikiana na watu ambao hawatumii akili au hawafikirii, yeye atakuwa mjinga zaidi kuliko wao. Kwa kiasi fulani ni vigumu

[8] Ni aina ya mti mgumu sana unaopatikana katika jamii ya Wachaga. Mti huu ndio unaotumika kutengeneza fito za kufungia ng'ombe katika nyumba za asili

[9] Aina ya pombe (mbege) iliyochanganyika na machicha ya pombe. Aina hii ya pombe haifai kwa matumizi ya binadamu.

kwa watu ambao si wenyeji wa maeneo ambako sitiari hii imeundwa kuweza kupata picha halisi kuhusu maana ya neno *mbulugha*. Aina hii ya pombe, haifai kabisa kunywa. Matumizi ya aina hii ya pombe yanawafanya wasomaji kupata picha halisi ya aina ya mwanamke aliyeolewa atakavyokuwa endapo ataandamana na watu ambao si wazuri katika jamii.

## 5.0 Hitimisho

Katika makala hii tumeangalia matumizi ya sitiari katika kazi za fasihi. Tumeona kuwa sitiari katika kazi za fasihi ni tamathali inayomsaidia msanii kueleza kwa kina yale aliyokusudia kuyafikisha kwa jamii kwa kutumia vitu mbalimbali ambavyo vinapatikana katika mazingira yanayomzunguka. Matumizi haya ya sitiari yanamwezesha msanii kutumia maneno machache kurejelea mambo mengi kwa wakati mmoja kulingana na kiwango chake cha ubunifu kuhusu mambo aliyoyaona, aliyoyasikia au kuyasoma kuhusu jamii.

Makala hii imetumia nyimbo tatu za taasisi ya ndoa kutoka katika jamii ya Wachaga wa Vunjo kuonesha sitiari zinavyotumika katika kazi za fasihi. Kutokana na nyimbo hizi tumebaini kuwa, watunzi wa kazi za fasihi huunda sitiari kutoka katika mazingira na maisha halisi ya jamii ambayo wahusika wameizoea. Hii inatokana na uwezo wa msanii kutumia vitu vinavyomzunguka kuunda sitiari kwa namna ya kuivuta hadhira huku zikiibua maudhui yaliyokusudiwa.

Aidha, kutokana na sitiari hizi kubuniwa ndani ya jamii kulingana na mazingira na utamaduni, ufafanuzi wake ni lazima kuzingatia utamaduni na mazingira hayo ili kupata kile kilichokusudiwa. Makala inashadidia hoja za Almirabi (2015) na Kövecses (2010), kuwa sitiari inapata maana katika mazingira husika au mahususi. Kwa hiyo, ni vigumu kuelewa sitiari fulani ina maana gani bila kuelewa mazingira ilimotumika (Bergmann, 1982; Lakoff na Johnson, 2003).

Kutokana na ujumbe uliotolewa kupitia nyimbo teule zilizochunguzwa, ni dhahiri kuwa fasihi ina jukumu na nafasi kubwa katika kufunza, kurekebisha, kukosoa na kutahadharisha jamii katika masuala mbalimbali. Pia, fasihi ina uwezo wa kuwaandaa wanajamii kukabiliana na maisha ya kila siku, mathalani, suala la kufanya kazi kwa bidii na maarifa, kujifunza mbinu za kukabiliana na matatizo yanayotokea katika jamii, kujiepusha na mambo yasiyofaa, na kadhalika. Mitazamo hii ikisisitizwa katika jamii kwa njia mbalimbali zikiwamo za kifasihi, kila mwanajamii ataelewa nafasi yake na wajibu wake na atakuwa na ujasiri wa kuona kuwa anaweza kufanya mambo mbalimbali. Kwa upande wa wanandoa, nyimbo hizi zinawapa mwanga na kujitambua kuwa wameingia katika mfumo mpya wa maisha ya kusaidiana na kutegemeana na wana wajibu wa kuhakikisha kuwa familia wanayoianzisha inaishi kwa amani na upendo kwani hakuna taifa bora bila familia bora. Hii ina maana kuwa familia imara inatengeneza taifa imara.

Kwa maneno mengine, kama familia zitakuwa legelege, uchumi wa familia utayumba na hii itasababisha taifa kuwa maskini na litategemea misaada ili kuweza kuwahudumia wananchi wake. Kwa hiyo, wasanii wana nafasi kubwa ya kuhakikisha kuwa wanabuni mbinu mbalimbali zinazohamasisha mabadiliko katika familia kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na hivyo kujenga taifa imara linalojitambua na kujitegemea.

**Marejeleo**


Almirabi, M. A. (2015). "When Metaphors Cross Cultures." *Journal of Language Teaching and Research.* 6 (1), 204-209.

Bergmann, M. (1982). "Metaphorical Assertions." *Philosophical Review.* 91 (2): *229-245.*

Besha, M.R. (1983). "Utayarishaji wa Vitabu vya Kufunzia Wageni Kiswahili." (Hakuna Mh.), *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili II: Uandishi na Uchapishaji.* Dar es Salaam: TUKI. Kur. 60 - 76.

Black, M. (1962). *Models and Metaphors: Studies in Language and Philosophy*. New York: Cornell University Press.

Buliba, F.A. na Kamau, N.G. (2016). "Ufafanuzi wa Vichocheo vya Migogoro ya Kindoa kama Vinavyosawiriwa katika Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*". *International Journal of Advanced Education and Research.* 1(9): 19-27.

Carter, R. (1989). "Directions in the Teaching and Study of English Stylistics." Katika M. Short (Mh.), *Reading, Analysis and Teaching Literature*. New York: Longman Inc. Kur. 10-21.

Chesaina, C. (1994). "Images of Women in African Oral Literature: A Case Study of Kalenjin and Maasai Oral Narratives." Katika A. Bukenya, W. M. Kabira, and O. Okombo (Wah.), *Understanding Oral Literature.* Nairobi: Nairobi University Press. Kur. 85-92).

Comer, R. J. (1995). *Abnormal Psychology*. New York: W.H. Freeman.

Culler, J. (1981). "The Problem of Metaphor." Katika T.E. Hope, B.W. Reid, R. Harris na G. Price (Wah.), *Language Meaning and Style*. New York: Leeds University Press. Kur. 5-20.

Dundas, C. (1968). *Kilimanjaro and Its People*. London: Frank Cass and Company Ltd.

Guthrie, M. (1967). *Comparative Bantu.* Farnborough: Gregg International Publishers Ltd.

Kahigi, K.K. na Mulokozi, M.M. (1982). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House, Ltd.

Kövecses, Z. (2010). "Metaphor and Culture." *Philologica.* 2 (2): 197-220.

Lakoff, G. na Johnson, M. (2003). *Metaphor we Live By*. Chicago. Chicago University Press.

Lan, C. (2005). *Cognitive Linguistics and Metaphoric Study*. Beijing: Foreign Language Teaching and Research Press.

Leech, G.N. (1991). *A Linguistic Guide to English Poetry.* New York: Longman Group Inc. Limited.

Perrine, L. (1987). *Sound and Sense: An Introduction to Poetry*. New York: Harcourt Brace Jovanovich Publishers.

Marealle, P.I. (2002). *Maisha ya Mchaga hapa Duniani na Ahera*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Martin, G.D. (1975). *Language*, *Truth and Poetry.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utanguizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU

Muzale, H.R.T. na Rugemalira, J.M. (2008). "Researching and Documenting the Languages of Tanzania." *Language Documentation and Conservation.* 2(1): 68-108.

Nurse, D. (1977). Language and History of Kilimanjaro, the Taita Hills and the Pare Mountains. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). University of Dar es Salaam.

Robert, S. (1966). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Nairobi: Kenya Litho Limited.

Senkoro, F.E.M.K. (1988). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Stahl, K.M. (1969). "The Chaga." Katika P.H. Gulliver (Mh.), *Tradition and Transition in East Africa Studies of the Tribal Element in the Modern Era*. London: Routledge & Kegan Paul Ltd. Kur. 209-222.

TUKI (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.

Weedon, C. (1997). *Feminist Practice and Poststructuralist Theory*. Oxford: Basil Blackwell.

Vansina, J. (1985). *Oral Traditon as History*. Nairobi: Heinemann.[10]

[10] Katika hatua za mwisho za uandishi wa makala hii, mwandishi alipata ufadhili kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, "Female Leaders Academic Publishing Support Programme (FLAPS), 2022".